

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam  
30 May 2009**

**Waliohudhuria**

Juma Ali Salehe Jongo  
Sudi Saidi Ramadhan  
Mohammed Samwely  
George Kabogo  
Hamadi Hatibu Bwaja  
Filbert Mbecha  
Juma Hassan Chibaya  
Selion Elieskia  
Shamte J Kigoma  
Kibwana Mohammad Msiga  
Husein Hamza Hamisi  
Athmani Mussa  
Jasper Kobora  
Dominata Rwechungura  
Edgar R Paulo  
Mussa Omari  
Paulo Atibu Hatibu

**Mradi wa Wamba**

Idadi ya wanafunzi waliojiandikisha ni 40. Idadi ya walimu watakao kwenda kufundisha ni sita pasipo kujali idadi ya wanafunzi kama itaongezeka kufikia sitini au kubakia idadi hiyo hiyo ya wanafunzi 40. Na tumekubaliana kwamba iwapo idadi ya wanafunzi haitafikia sitini basi walimu watakaopata nafasi hii wawe tayari kumalizia mafunzo kwa wanafunzi watakao baika wakati wowote siku zijazo kwa malipo haya ambyo tutakuwa tumeshapata kwa awamu hii. Ni kukamilisha idadi ya wanafunzi sitini kwa hiyo orodha ya mahudhuria ya mkutano huu wote kwa pamoja tumkubaliana kwa hilo.

Nafasi ya walimu ambao wapo tayari kwenda kufundisha na hawajawahi kupata nafasi ya kwenda kufundisha ni: Mussa Omari, Kibwana Mohammed, Juma S Jongo.

Dominata Rwechungura amepitishwa bila kupigiwa kura ni nafasi pekee kwa mwalimu mwanamke.

Uchaguzi ulifanyika kati ya watu watano. Filbert Mbecha (na Hamadi Bwaja) walichaguliwa na Mohammed Samweli, Edgar Paulo na Paulo Hatibu hawajachaguliwa.

Kwa hiyo hawa ndoo walimu watakaokwenda kufundisha: Mussa Omary, Kibwana Mohammed, Juma S Jongo, Dominata Rwechungura, Filbert Mbecha, Hamad Bwaja.

**JICA**

JICA wametualika kwenye mkutano jumatatu. Wanachama wafuatao ndio watakao hudhuria mkutano na JICA tarehe 1/6/09 siku ya jumatatu: Hamad Bwaja, Hussein Hamza, Mussa Omary.

### **Mkutano wa Tanga**

Taarifa ya mkutano wa Tanga kutoka kwa mwanachama mwakilishi Dominata Rwechungura – Alipata nafasi ya kusimama na kuelezea suala zima kuhusu baisikeli, kuhusu njia salama za wapanda baisikeli na kuendesha kwa kufuata sheria na ni baada ya kuteuliwa kutoka katika kazoo za makundi. Wengi wao walifuatalia kazoo nzuri zinazofanywa na UWABA na Meya wa Jiji la Tanga amefurahi sana kwahilo na ameahidi atajitahidi kutenga bajeti kwa ajili ya UWABA ili wakatoe mafunza kwa wapanda baisikeli mkoani Tanga kwa siku zijazo.

Dominata Rwechungura alipata wazo binafsi alimpa jacket reflecter na helmet na meya wa Tanga, ni suala ambalo liliweza kuleta hamasa zaidi kutoka UWABA kwani aliweza kuitoa kwa niaba ya UWABA.

### **Mambo ya hela na guta**

Dereva hajaleta pesa, kwa hiyo anadaiwa Tsh 7,000 ya wiki hii.

Mtunza fedha ndogondogo Filbert Mbecha ana pesa ya chama Tsh 3,000 na pesa ya mradi wa Wamba Tsh 30,000, jumla ana Tsh 33,000.